

**MKATABA WA UPANGAJI WA ENEO LILILOPO KWENYE KIWANJA  
NAMBA 1649 KONGOWE, HALMASHAURI YA MJI KIBAHA  
MATUMIZI YA KITUO CHA MAFUTA NA ENEO LA KUPAKI MAGARI**

Makubaliano haya yamefanyika leo Tarehe **11** Mwezi wa **04** Mwaka **2021**

**KATI YA**

**TAWAQAL & CO LIMITED** wa S.L.P **106284** DAR ES SALAAM mwenye namba ya simu (Ambaye katika mkataba huu anaitwa “**Mmiliki**”) kwa upande mwingine.

**NA**

**SUDENERGY LOGISTICS COMPANY TANZANIA LIMITED** wa S.L.P **106284** DAR ES SALAAM (Ambaye katika mkataba huu anaitwa “**Mpangaji**”)

**KWA KUWA ;.**

- a) Mmiliki anakubali kupangisha kiwanja namba 1649 Kongowe Halmashauri ya Mji Kibaha kwa kipindi cha **Miaka Mitano** kuanzia tarehe **11** mwezi wa **04** mwaka **2021** hadi tarehe **10** mwezi wa **04** mwaka **2026** kwa matumizi tajwa hapo juu na kwa mashariti yaliyoainishwa hapo chini .
- b) Mpangaji ameonyesha na kuthibitisha nia na uwezo wa kupanga eneo hili **kwa** ajili ya matumizi ya kituo cha mafuta na eneo la kupaki magari kwa mashariti yaliyoainishwa ndani ya mkataba huu:

**MKATABA HUU UNASHUHUDIA NA KUTHIBITISHA YAFUATAYO:**

- 1) Kodi ya eneo ni **Tshs 500,000/=** tu kwa mwezi kutokana na makubaliano ya pande zote mbili ambayo italipwa kwa awamu nne ndani ya mwaka (**miezi mitatu kila awamu**)
- 2) Mwenye kiwanja amemkabidhi mpangaji eneo na pande zote zinakubaliana kuwa kipindi cha mkataba huu, yaani **Miaka Mitano** kimeanza kuhesabiwa rasmi tarehe **11** mwezi wa **04** mwaka **2021**
- 3) Mpangaji anaahidi na kumthibitisha mwenye eneo kwamba:
  - a) Atalipa kodi iliyotajwa hapo juu bila makato ya aina yoyote.
  - b) Ataweka na kutunza eneo alilopangisha na mazingira yake katika hali nzuri na safi kwa muda wote atakaokuwa amepanga,

- c) Mpangaji ataruhusiwa kufanya mabadiliko au ongezeko lolote kwenye eneo yanayohusu miundombinu ya kudumu kama ujenzi.
  - d) Mpangaji atatumia eneo hilo kwa ajili ya matumizi yaliyoainishwa hapo juu.
  - f) Atatii sheria zote za usafi ,Afya zinazotolewa na Halmashauri ya jiji na vyombo vya dola kuhusiana na namna ya kuliendeleza Eneo hilo.
  - g) Hataruhusiwa kumpangisha /Kumrithisha nyumba /Eneo mtu mwingine yeyote bila idhini ya mwenye nyumba/Eneo kwa maandishi.
- 4) Mwenye eneo anaahidi na kumthibitishia mpangaji kwamba:
- a) Ataweka eneo analopangisha katika hali nzuri kwa ajili ya kupangisha.
  - b) Atampangisha mpangaji eneo kwa ajili ya matumizi yaliyoainishwa hapo juu.
  - c) Endapo mpangaji atalipa kodi iliyokubalika na atatimiza masharti yote ya mkataba huu, mwenye eneo atamwacha huru kutumia Eneo bila kero ,fedhea , bughudha au usumbufu wowote kutoka kwa anayedai kwamba ana haki au uhusiano utokanao na mwenye eneo.
- 5) Pande zote mbili zinakubaliana kama ifuatavyo:
- a) Mwenye eneo au mpangaji ana haki ya kuvunja mkataba huu kwa kutoa taarifa ya miezi mitatu kwa maandishi .Endapo mwenye eneo atavunja mkataba kwa mujibu wa kifungu hiki basi atarudisha kodi ya pango ya kipindi kilichobaki baada ya kuvunja mkataba.
  - b) Endapo mpangaji atavunja mkataba kwa mujibu wa kifungu hiki mwenye nyumba hatawajibika kurudisha kodi ila pande zote zitashirikiana na kutafuta mpangaji mwingine anayekubalika na mwenye eneo na mpangaji atapata fedha yake toka kodi iliyolipwa na mpangaji mpia.
  - c) Mpangaji anaweza kuendeleza/kutoendeleza mkataba huu kwa kipindi kingine cha mwaka mmoja endapo mpangaji atampa mwenye eneo taarifa (notice) ya miezi mitatu (3) kwa maandishi kabla ya mkataba huu kumalizika kwamba anahitaji kuendeleza mkataba huu au vinginevyo endapo mwenye eneo na mpangaji watakubaliana kuhusu kiasi cha kodi kitakacholipwa. Na bila kutoa taarifa ndani ya kipindi hicho cha miezi mitatu mara tu ya tarehe ya mkataba kuisha mpangaji atatakiwa kukabidhi Nyumba/Eneo kwa mpangishaji.

Kwa kushuhudia na kuthibitisha hayo tumeweka sahihi zetu hapa chini leo tarehe **01.mwezi 04** mwaka **2021**

**SEHEMU YA MMILIKI WA ENEO**

Umetolewa na kusainiwa tarehe 10/04/2021

Jina la mmiliki /msimamizi **Aziz Mohammed Soud**

Sahihi .....

**SEHEMU YA MPANGAJI WA ENEO**

Jina la Mpangaji **SUDENERGY LOGISTICS COMPANY TANZANIA LIMITED**

Sahihi .....

Umetolewa na kusainiwa tarehe **10/04/2021**



**MBELE YA SHAHIDI**

Jina .....

Cheo .....

Sahihi .....

Tarehe .....

